




# Swahili Colloquium Bayreuth



UNIVERSITÄT  
BAYREUTH

## 32<sup>nd</sup> SWAHILI COLLOQUIUM in Bayreuth, from 31<sup>st</sup> May until 2<sup>nd</sup> June 2019

Tarehe 1 Aprili 2019

Waalikwa Wapendwa – Mabibi na Mabwana,

Kwa mara nyingine tunawashukuruni sana kwa kuuitika mwito wetu. Kwa furaha tumepokea mihtasari na makala yenu nyingi. Kukutana nanyi nyote hapa kwetu itakuwa furaha hata zaidi. Karibuni sana!

Katika barua hii ya pili tunawatumia pia ratiba ya kongamano la mwaka huu, kama ilivyo kwa wakati huu. Kongamano la mwaka huu litafanyika *Iwalewahaus*. Anwani ni: Iwalewahaus, Wölfelstr. 2, 95444 Bayreuth. Kongamano litaanza **Ijumaa tarehe 31**, saa mbili na nusu asubuhi. Kujisajili kutagharimu Euro 15 kwa wasio wanafunzi / Euro 10 kwa wanafunzi wageni.

Siku moja kabla ya Kongamano, yaani **Alhamisi tarehe 30**, saa moja, tutakutana kwa chakula cha jioni kama ilivyo kawaida yetu. Mkahawa unaitwa ‘Hua Hin’ (anwani: Ludwigstr. 30; <http://www.thai-huahin.de/>). Tafadhali muelewe kwamba hatuwezi kulipa siku hiyo.

Bali na hayo kongamano letu lina mambo ya zaida: **Jumamosi** jioni kwa furaha kubwa tutawakaribisha washindi wa kwanza wa tuzo la Mabati-Cornell (Mabati Cornell Kiswahili Prize for African Literature [<http://kiswahiliprize.cornell.edu/>]). Kwa upande wa riwaya, Zainab Alwi Baharoon atasoma kutoka riwaya yake “Mungu Hakopeshwi” na kwa upande wa ushairi, Jacob Ngumbau Julius atasoma baadhi ya mashairi ya diwani yake “Moto wa Kifuu”.

Tutakuwa na panel moja yenye anwani ““Sociolinguistic variation and change in Kiswahili: Creative practices, playful language, translocal communication” inayoandaliwa na Nico Nassenstein (Mainz) na Andrea Hollington (Cologne). Na pia tutakuwa na panel inayoandaliwa na Annachaira Raia (Leiden) na Clarissa Vierke (Bayreuth) itakayohusu: “Baina Pwani na Bahari: Indian Ocean Networks”.

Vilevile wakati wa kongamano tutakuwa na kumbukumbu ya mtalamu wa kipekee, marehemu Elena Bertoncini Zúbková, aliyeaga dunia muda si mrefu.

Kama una maswali yoyote ya zaida, usisite kuwasiliana nasi. Anwani ni: [swahili@uni-bayreuth.de](mailto:swahili@uni-bayreuth.de)

Karibuni sana!

Salamu nyingi,

Clarissa Vierke, Nikitta Adjirakor, Serena Talento, Duncan Tarrant